# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR



## MHE. DKT HUSSEIN ALI HASSAN MWINYI
## RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
## WA BARAZA LA MAPINDUZI

YALIYOMO

A. UTANGULIZI ........................................................ 1
B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 .......................... 6
E06: Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ........................................................... 7
Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma ............................................ 7
Programu ya Huduma za Serikali Mtandao ........... 9
Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora ............ 10
Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais,Utumishi wa Umma na Utawala Bora ....... 11
Uratibu wa Usimamizi wa Miradi ya Wizara .......... 14
Usimamizi wa Usalama wa Watumishi wa Umma ....15
TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU ........................ 16
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ............... 17
Chuo cha Utawala wa Umma ............................. 19
Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ................ 21
A02: AFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI .............. 22
Programu ya Uratibu wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi ..................... 22
Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria...... 23
Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini ........ 25
E04: OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.......................................... 27
Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa fedha na Rasilimali za Umma .......................................... 27
EO5: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ........................................................ 28
Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. .................................. 28
E07: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA ................. 30
Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma 30
E08: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI ........................ 32

Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini ..................... 32
G02: MAHKAMA KUU ................................................ 33
Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki .. 33
G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU ......................... 35
Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa huduma za Sheria.................................................................... 35
G04: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ............. 37
Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai ......................................................... 37
G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ....................... 38
Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria ..... 38
C. MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 ........................................... 41
D. VIPAUMBELE VYA OFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 ............................................ 42
MALENGO MAKUU YA OFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 ...................................... 43
G01: AFISI YA RAIS- KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA ........................................... 45
Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria ..... 45
Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini......... 46
Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora ........... 47
Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma ........................................... 48
Programu ya Huduma za Serikali Mtandao .......... 49
Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ARKSUUB 50
TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU- G01 ................ 53
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ............... 53
Chuo cha Utawala wa Umma ............................. 54
Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ................ 55
A02: AFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI .............. 55
Programu ya Uratibu wa Majukumu Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi. ..................... 55
G02: MAHKAMA KUU ................................................ 56

Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki ............ 56
G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU ............ 57
Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria ............ 57
G04: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ............ 58
Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai ............ 58
G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ............ 59
Programu ya Usimamizi wa mapitio ya Sheria ..59
E04: AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ............ 60
Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa fedha na Rasilimali za Umma ............ 60
E05: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ............ 60
Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rusha na Uhujumu Uchumi ............ 60
E07: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA ............ 61
Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma ............ 61
E08: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI ............ 62
Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki, na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini ............ 62
E. SHUKRANI ............ 63
F. HITIMISHO ............ 65
Kiambatanisho namb. 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha 2020/2021(katika, 000) 67
Kiambatanisho namb. 2:Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2021/2022 (katika, 000) ............ 75
Kiambatanisho namb. 3: Makusanyo ya Mapato Julai / Machi 2020/2021 na Makadirio ya Mwaka 2021/2022 ............ 92
Kiambatanisho namb. 4: Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo kwa kipindi cha

Julai-Machi 2020/2021 ........................................ 93
Kiambatanisho namb. 5a: Mafunzo ya Watumishi wa Ofisi Muda Mrefu na Mfupi .......... 95
Kiambatanisho namb. 5b: Tuhuma za Rushwa kwa Kipindi cha Julai /Machi 2020/2021 ........... 98
Kiambatanisho namb 6a: Watumishi walioajiriwa kuanzia Julai, 2020 hadi Kufika Machi, 2021 ............................................100
Kiambatanisho namb. 6b: Shughuli za Tume ya Utumishi Serikalini kuanzia Julai, 2020 hadi kufika Machi, 2021 ..............................................102
Kiambatanisho namb. 6c: Malalamiko ya Watumishi kuanzia Julai 2020 hadi kufikia Machi 2021........................................................104
Kiambatanisho namb. 7a: Ufunguaji wa Kesi katika Mahkama mbali mbali Julai 2020 hadi Machi 2021........................................................ 105
Kiambatanisho namb. 7b: Ufunguaji wa Kesi katika Mahkama za Mwanzo Julai 2020 hadi Machi 2021 ...................................................... 107
Kiambatanisho namb. 7c: Ufunguaji wa kesi katika Mahkama za Kadhi wa Wilaya Julai 2017 hadi Machi 2018 ................................................ 107
Kiambatanisho namb. 8: Matangazo ya Kisheria ya; Afisi ya Mwanasheria Mkuu ................................. 109

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati, ili liweze kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii kwa ajili ya kuwasilisha taarifa ya utelekezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 na mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kutuwezesha kutekeleza vyema mipango na malengo tuliojipangia ya kuwahudumia wananchi.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza kwa dhati na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar na kuimarisha amani na utulivu. Tunamuomba

Mwenyezi Mungu ampe nguvu, afya njema na umri mrefu Rais wetu ili aendelee na majukumu yake ya kuiongoza Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika**, niruhusu pia nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Othman Masoud Othman kwa kuridhia kuteuliwa kwake kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais Zanzibar na kumsaidia Mhe. Rais katika utekelezaji wa majukumu ya kuiongoza nchi yetu.

5. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdalla, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kwa namna anavyomsaidia na kumshauri kwa hekima Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na kusimamia na kuratibu shughuli za kila siku za Serikali katika Baraza la Wawakilishi.

6. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika, kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza la Wawakilishi kwa umakini, busara na hekima kubwa. Nawapongeza pia, Wenyeviti wa Baraza kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuliongoza Baraza letu Tukufu na kusimamia kanuni tulizojiwekea.

7. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee nampongeza Mheshimiwa Hassan Khamis

Hafidh, Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi na Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Welezo, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mtumwa Peya Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Bumbwini na Wajumbe wote wa Kamati kwa maelekezo na mashirikiano mazuri wanayotupatia katika kukamilisha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021 na maandalizi ya bajeti ya mwaka 2021/2022 na kuongeza ufanisi wa utekelezaji. Ni imani yangu kuwa tutaendelea kushirikiana nao vyema katika utekelezaji wa majukumu yetu tuliokabidhiwa.

8. **Mheshimiwa Spika,** nawapongeza pia, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali (PAC) Mheshimiwa Juma Ali Khatib na Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa (Kwaza) Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa mashirikiano yao mazuri ya kikazi na Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

9. **Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Wawakilishi wote kwa kuchaguliwa kuwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na kuanza vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na kwa ushirikiano mzuri wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu nikiwa

Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Kipekee napenda kuishukuru familia yangu na wapiga kura wa Jimbo la Uchaguzi la Makunduchi ambao wameendelea kunionyesha upendo na imani kwa kunichagua kwa mara nyengine tena kuwa Muwakilishi wao ili niendelee kuwawakilisha katika chombo hiki na kuwaletea maendeleo. Niahidi kwamba nitaendelea kushirikiana nao na wasiwe na wasiwasi tutaendelea kuwatumikia kwa nguvu zetu zote na kuhakikisha Jimbo la Makunduchi linakuwa mfano hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

**10.** **Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzangu wote, Viongozi na Wanachama wa Chama changu cha Mapinduzi kwa msiba mzito uliotokea tarehe 17 Machi 2021, wa kuondokewa na aliekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi taifa. Ni Dhahiri kuwa taifa letu limempoteza shujaa na kiongozi jasiri na mzalendo aliejitolea kwa nguvu zake zote kupiga vita vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma na kuhakikisha kuwa nidhamu na uwajibikaji wa watumishi wa umma vinaimarishwa katika utekelezaji wa majukumu ya kuwahudumia wananchi. Tumuombe Mwenyezi Mungu aipumzishe roho ya Marehemu mahali pema na aijaalie Amani na utulivu nchi yetu. Aidha, natoa pole kwa

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wanachama wa Chama cha ACT Wazalendo na wananchi wote wa Zanzibar kwa kifo cha Maalim Seif Sharif Hamad, aliekuwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo.

11. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia jumla ya mafungu matano ya iliokuwa Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambayo ni; **E06-** Ofisi Kuu; **E04**- Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na **E05**- Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi; **E07**- Kamisheni ya Utumishi wa Umma; na **E08** Tume ya Utumishi Serikalini.

12. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na mabadiliko ya Wizara yaliofanywa hivi karibuni ya kuunganisha majukumu ya Sekta ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Sekta ya Sheria baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa Oktoba 2020, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia pia, mafungu **G02-** Mahkama Kuu; **G03**- Afisi ya Mwanasheria Mkuu; **G04**- Mkurugenzi wa Mashtaka na **G05**- Tume ya Kurekebisha Sheria kutoka iliokuwa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na fungu **A02**- Afisi ya Rais Baraza la Mapinduzi. Vile vile, Afisi hii inasimamia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Tume ya Maadili ya Viongozi

wa Umma na Chuo Cha Utawala wa Umma (IPA) kupitia ruzuku inayotolewa.

**13. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa naomba kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/2021 na mwelekeo wa bajeti ya mwaka 2021/2022 kama ifuatavyo.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**14. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ilipanga kutumia jumla ya Shilingi 33,707,371,340 kutoka kwa iliokuwa Ofisi ya Rais- Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Katiba na Sheria kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 25,068,571,340 zimepangwa kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida, shilingi 3,500,000,000 zimepangwa kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo na shilingi 5,138,800,000 ni ruzuku kwa ajili ya taasisi zinazopokea ruzuku kutoka Serikalini.

**15. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi 2021, jumla ya Shilingi 8,294,184,667 zimepatikana sawa na asilimia 27.5 ya bajeti kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na matumizi mengineyo. (**angalia viambatanisho namb. 1&2**).

Kwa upande wa kazi za maendeleo Shilingi 317,642,000 zimepatikana sawa na asilimia 9. Pia, Ofisi ilikusanya Shilingi 88,930,000 sawa na asilimia 56 (**angalia viambatanisho namb. 1& 3).**

### E06 - Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

**16.** **Mheshimiwa Spika,** Fungu la **E06** linahusisha Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma; Programu ya Huduma za Serikali Mtandao; Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Idara taasisi zinazosimamiwa na Katibu Mkuu.

**17.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2021, hatua za utekelezaji wa programu za Fungu **E06** ni kama ifuatavyo:-

### Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma

**18.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya usimamizi na uendelezaji wa Watumishi wa Umma ina programu ndogo mbili zinazotekelezwa kupitia Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi.

19. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango ya Raslimaliwatu kupitia programu hii imefanikiwa kutoa elimu ya utayarishaji wa Mpango wa Raslimali watu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa watendaji na watumishi wa Wizara, Idara, Taasisi zinazojitegemea na kufanya vikao vya majadiliano na Taasisi za Umma kubainisha watumishi waliopo katika Utumishi na mahitaji ya nafasi mpya zinazohitajika katika Utumishi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Idara imetoa vibali vya uhamisho wa watumishi kutoka taasisi mbali mbali za Serikali na kuwajengea uwezo watumishi tisa (9) wakiwemo wanaume watano (5) na wanawake wanne (4) kwa kupewa nafasi za masomo nje ya nchi kupitia Ubalozi wa Korea nchini Tanzania.

20. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi 338,164,000 na hadi kufikia Machi 2021, jumla ya Shilingi 157,883,630 zimepatikana sawa na asilimia 47.

21. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi kupitia programu ya Miundo na Mifumo ya Taasisi imefanya mapitio ya Miundo ya Utumishi ya Mawizara 16 na kuiwasilisha Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kuidhinishwa. Idara pia, imefanya uhakiki wa mishahara na Maposho katika Taasisi na Wizara za Serikali, kuendelea kutoa Miongozo na Matoleo mbali mbali ya kiutumishi na kufanya marekebisho

ya Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011 ambayo imewasilishwa Tume ya Kurekebisha Sheria kwa tathmini zaidi.

22. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 378,248,000 na hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 188,586,330 zimepatikana sawa na asilimia 50 kwa matumizi ya mshahara na matumizi mengineyo.

**Programu ya Huduma za Serikali Mtandao.**

23. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali Mtandao kupitia programu hii imekamilisha Muundo wa Wakala wa Serikali Mtandao na kuwasilishwa Serikalini kwa ajili ya kuidhinishwa. Wakala imefanya matayarisho ya awali ya rasimu ya kanuni za TEHAMA na Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Serikali Mtandao (e-Government Strategy) na kuandaa nyaraka za mahitaji ya Mfumo wa Mamlaka ya Utoaji Leseni na mfumo wa maombi ya ajira kwa Tume ya Utumishi Serikalini.

Vile vile, Wakala imefanya mapitio ya nyaraka za Miradi ya TEHAMA ya Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) na uanzishaji wa mfumo wa Usimamizi wa Bandari na kutoa ushauri wa kitaaalamu. Pia, Wakala imesimamia mradi wa utengenezaji wa mfumo wa mapato ya Serikali (Zanzibar electronic Payment Gateway – ZanMalipo) na mradi wa uwekaji wa taarifa za

maendeleo ya watumishi na mshahara (Integrated Human Resource and Payroll System). Aidha, mfumo wa Barua pepe za uwekaji wa tovuti umefanyiwa tathmini na kuimarishwa pamoja na kufanya tathmini ya miundo ya ndani "LAN" ya utoaji wa huduma za mtandao "internet" kwa taasisi 10 za Umma.

24. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mafunzo ya watumishi, Watendaji wawili wa Wakala wamepatiwa mafunzo ya udhibiti wa mifumo ya kielektroniki "DNSSEC (Domain name System Security Extension).

25. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 686,596,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 278,498,645 zimepatikana sawa na asilimia 41 kwa matumizi ya mshahara na matumizi mengineyo.

**Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora**

26. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2021, Idara ya Utawala Bora kupitia programu ya usimamizi wa utawala bora imefanya mikutano miwili ya uhamasishaji wa masuala ya utawala bora kwa jamii na kuwapatia elimu ya utawala bora wananchi 600 kupitia makongamano ya utawala bora yaliofanyika Unguja na Pemba. Idara imetayarisha na kurusha hewani vipindi 50 vya utawala bora kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar na redio Jamii ya Mkoani na Micheweni

Pemba na kutoa maelezo baada ya habari 7 kuhusu uzingatiaji wa matakwa ya wananchi na utekelezaji wa maagizo ya Serikali.

Idara pia, imetayarisha Jarida la utawala bora toleo la 4 la mwaka 2020 na kusambaza nakala 833 kwa wahusika pamoja na kuwapatia elimu ya utawala bora wananchi 491 waliotembelea banda la utawala bora katika maonesho ya kuadhimisha sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2021. Aidha, wanafunzi 18 wa Serikali ya wanafunzi katika Chuo cha Zanzibar School of Health nao walipata fursa hiyo.

27. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 255,920,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 120,481,455 zimepatikana sawa na asilimia 47 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

### Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

28. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina programu ndogo tatu ambazo ni;- programu ya Uongozi na Utawala, programu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti na programu ya Uratibu wa Shughuli za Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Pemba zinazotekelezwa kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango Sera na Utafiti na Afisi Kuu Pemba. Programu hii pia, inajumuisha programu ndogo ya kusimamia

usalama wa watumishi inayotekelezwa na Idara ya Usalama wa Serikali.

**29.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2021, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia programu ya Uongozi na Utawala imeshughulikia upatikanaji wa huduma ya maji, umeme, ununuzi wa vifaa na kufanya matengenezo ya kompyuta 12, vipoza hewa na "lift" mbili. Idara pia, imefanya uchambuzi wa Kumbukumbu za Wizara na kuhifadhi mafaili 506 kwenye maboksi 82 na kumbukumbu muhimu za Serikali katika Kituo cha Kuhifadhia Kumbukumbu kwenye Kitengo cha TEHAMA.

Kwa upande wa maslahi ya watumishi, jumla ya watumishi 55 waliopimwa utendaji kazi wao wamelipwa nyongeza ya mshahara, watumishi 30 wamelipwa posho la likizo, 31 malipo baada ya saa za kazi na watumishi saba (7) wamepatiwa ubani wa kufiwa na watu wao wa karibu. Aidha, mafunzo ya matumizi ya barua pepe za Afisi na uingizaji wa taarifa za kielektroniki za wafanyakazi katika Mfumo wa Uhifadhi wa Kumbukumbu za Watumishi "HRIS -Data base" yametolewa kwa watumishi husika.

**30.** **Mheshimiwa Spika,** Idara imeandaa Mpango wa Rasilimali Watu wa Mwaka 2021/2022 ili kutoa mahitaji halisi ya watumishi wa Wizara, kutayarisha Mpango wa Ukaguzi wa Ndani wa Wizara wa mwaka na kutoa ripoti ya ukaguzi wa robo ya tatu. Vile vile, Idara imeratibu vikao vya

Kamati Tendaji, Kamati ya Uongozi na vikao vya kupeana taarifa vya kila wiki.

31. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi 1,358,111,000 na hadi kufikia Machi 2021, jumla ya Shilingi 707,388,585 zimepatikana sawa na asilimia 52 kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

32. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2021 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti imeratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera, Mipango na Bajeti ya Wizara, kutayarisha ripoti za utekelezaji wa majukumu ya sekta za robo na nusu mwaka na kutayarisha Bajeti na Mpango wa mwaka 2021/2022.

Idara imeandaa Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Malipo ya Watumishi wa Umma na Wanasiasa ya mwaka 2019 na kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara na Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya kuandaa mipango mipya ya Ufuatiliaji na Tathmini na Mpango Mkakati kwa mujibu wa muundo na majukumu ya sasa ya Wizara.

Kwa upande wa utafiti, matayarisho ya utafiti wa Hali ya Rushwa na Utawala Bora yamekamilika na hatua za ukusanyaji wa taarifa za utafiti huo zinaendelea.

33. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 350,165,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 132,590,560 zimepatikana

sawa na asilimia 51 kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

**Uratibu wa Usimamizi wa Miradi ya Wizara**

34. **Mheshimiwa Spika,** Idara kwa kushirikiana na taasisi husika imeratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ifuatayo:

- Mradi wa Awamu ya Pili ya Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma;
- Mradi wa Ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi;
- Mradi wa Uwezeshaji wa Kisheria na Upatikanaji wa Haki; na
- Mradi wa Ujenzi wa Skuli ya Sheria.

35. **Mheshimiwa Spika**, hatua za utekelezaji wa miradi hiyo ni kwamba kazi za usanifu na uandaaji wa michoro ya jengo la Skuli ya Sheria zinaendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi zimekamilika. Aidha, utekelezaji wa kazi za mradi wa Uwezeshaji wa Kisheria na Upatikanaji wa Haki umeendelea kwa hatua mbali mbali ikiwemo uchapishaji wa nakala 500 za Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na marekebisho yake na kuzigawa katika taasisi mbali mbali za Serikali, uchapishaji wa nakala 150 za Ripoti ya Mwaka ya Msaada wa Kisheria na nakala 125 za Ripoti ya Awali ya Hali Halisi ya Msaada wa Kisheria pamoja na kutoa

mafunzo ya Utatuzi wa Migogoro na Usuluhishi (Mediation and Arbitration) kwa Wanasheria 35 kutoka taasisi mbali mbali za Serikali.

36. **Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa jengo la Mahkama Kuu Tunguu umefikia asilimia 80 ya utekelezaji wa jumla hadi kufikia Machi 2021. Kama mambo yatakwenda vizuri, mradi huu unatarajiwa kukamilika mapema mwezi Juni 2021.

**Usimamizi wa Usalama wa Watumishi wa Umma**

37. **Mheshimiwa Spika,** programu ya Usimamizi wa Usalama wa watumishi wa umma inayotekelezwa na Idara ya Usalama wa Serikali imefanya upekuzi kwa watumishi 2,144 sawa na asilimia 79 ya lengo kutoka katika Wizara na taasisi mbali mbali za Serikali. Kati ya hao, watumishi 1,882 walifanyiwa upekuzi wa awali na watumishi 262 walifanyiwa upekuzi maalum. Idara pia, imefanya ukaguzi wa kiusalama katika jengo na maeneo ya utunzaji wa nyaraka katika Afisi ya Tume ya Utumishi Serikalini, Ikulu ndogo Kibweni na Chuo Cha Utawala wa Umma- IPA na kutoa ushauri.

38. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi 200,598,000 na hadi kufikia Machi 2021, jumla ya Shilingi 32,515,000 zimepatikana sawa na asilimia 20 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

39. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2021, programu ya Uratibu wa shughuli za Afisi imeratibu na kusimamia shughuli za utawala, utumishi na mipango ya Ofisi kwa upande wa Pemba kwa kufanikisha vikao sita (6) na Watendaji Wakuu wa Taasisi ziliomo katika Wizara vyenye lengo la kuwataka watumishi hao kusimamia na kutekeleza vyema majukumu yao ya kazi waliopangiwa kwa mujibu wa sheria na miongozo ya kiutumishi. Aidha, ofisi imefuatilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi za Wizara ziliopo Pemba na kuhimiza uwajibikaji wa watumishi katika utoaji huduma bora kwa wananchi kwa kuzingatia mkataba wa huduma kwa umma. Vile vile, mafunzo ya ndani kuhusu utunzaji wa kumbukumbu na masuala mtambuka (crosscutting issues) yametolewa kwa watumishi wa ofisi, kwa ajili ya kuwawezesha watumishi hao kutunza vyema kumbukumbu za Serikali na kupima afya zao.

40. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 539,865,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 319,187,000 zimepatikana sawa na asilimia 59.

**TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU.**

41. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo inayotolewa kwa taasisi tatu (3) zinazopokea

ruzuku kupitia afisi hii kwa ajili ya utekelezaji wa program ziliomo katika taasisi hizo. Taasisi zenyewe ni:- Chuo Cha Utawala wa Umma, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kamisheni ya Waqfu na Mali ya Amana. Utekelezaji wa kazi katika taasisi hizo ni kama ifuatavyo: -

**Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana**

42. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 jumla ya tirka 1,050 zimefunguliwa, kati ya hizo, tirka 984 sawa na asilimia 94 zimefunguliwa Unguja na tirka 433 sawa na asilimia 41 kwa upande wa Pemba. Aidha, jumla ya tirka 1,512 zimefungwa kati ya 1,734 zilizopangwa sawa na asilimia 87.1 (1,086 Unguja sawa na asilimia 72 na 426 Pemba sawa asilimia 28). Kati ya tirka 1,086 zilizofungwa Unguja, 562 ni kongwe na tirka 524 ni mpya na tirka 426 zilizofungwa Pemba 79 ni kongwe na tirka 347 ni mpya.

Kwa upande wa shughuli za mirathi, jumla ya mali yenye thamani ya Shilingi 35,112,894,210.92 (Unguja TZS 33,180,979,219.18 na TZS 1,931,914,991.74 kwa Pemba) kati ya Shilingi 16,290,000,000 iliyokisiwa imerithishwa kwa wananchi.

43. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya kesi 111 zimesimamiwa katika Mahkama mbali mbali za Unguja na 15 ni katika mahkama ziliopo Pemba. Kati ya kesi hizo, sita (6) ni za kushtaki, kesi sita

(6) ni za kushtakiwa na 99 ni za kushirikishwa. Pia, mizozo 32 imepatiwa ufumbuzi na 39 inaendelea kushughulikiwa kati ya mizozo 71 iliyoshughulikiwa katika kipindi hicho. Jumla ya mashauri 122 yamepatiwa ushauri wa kisheria (68 Unguja na 54 Pemba). Aidha, utekelezaji wa mradi wa kuanzisha Mfumo wa Mirathi kieletroniki unaolenga kutumia mtandao katika kutoa huduma za mirathi kwa Unguja na Pemba umefikia asilimia 96 ya utekelezaji na mapendekezo ya Mswaada wa Sheria mpya ya Kamisheni ya Wakfu yanaendelea kufanyiwa kazi.

44. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki jumla ya nyakfu 22 mpya zimesajiliwa, mashamba 10 na Nyumba 420 yamekaguliwa. Kati ya nyumba zilizokaguliwa, 123 haziridhishi na kuhitaji kufanyiwa marekebisho ya haraka, nyumba 200 zipo katika hali ya wastani na 97 zipo katika hali nzuri.

Jumla ya Shilingi 541,512,910 za kodi ya nyumba za Wakfu, amana na mashamba zimekusanywa na Shilingi 106,511,662.1 zimetumika kufanyia matengenezo katika nyumba kumi (10) ikiwa ni fedha za nyakfu husika.

45. **Mheshimiwa Spika,** naomba nitoe tahadhari kwa wale wote waliokodishwa nyumba hizi na kufunga Mikataba nao kuwa ni makosa kwa mujibu wa sheria nam. 2 ya mwaka 2007 kukodisha nyumba hizo kwa watu wengine zaidi ya wao wenyewe. Nitoe wito waliokodishwa

nyumba hizo na watu waliokodishwa kuwa Serikali itachukua hatua ambazo itampa haki yule anaekaa sasa hivi.

46. **Mheshimiwa Spika,** maandalizi ya Hijja kwa mwaka 2021 bado yanaendelea ingawa bado Serikali ya Saudi Arabia haijatoa muongozo rasmi wa Hijja kwa mwaka huu. Ili kuwa na utaratibu mzuri wa utekelezaji wa Hijja tayari Baraza la Mapinduzi limeshaidhinisha kuanzishwa kwa Mfuko wa Hijja hapa Zanzibar na maandalizi yote ikiwemo kuandaa Afisi, watendaji, vifaa na Mfumo wa kielektroniki wa Hijja yameshafanyika. Uandaaji wa Kanuni za Hijja, Umra na ziara zimeshatangazwa katika Gazeti rasmi la Serikali na kuanza kutumika. Jumla ya vipindi 22 vimerushwa hewani kupitia ZBC Redio na Televisheni, kuchapisha vipeperushi 1,220 na kugawiwa kwa wananchi na kuandaa makala mbili kwa ajili ya kuelimisha wananchi.

47. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 872,539,384 na hadi kufikia Machi 2021, jumla ya Shilingi 462,677,867 zimepatikana kwa ajili ya mishahara na Shilingi 116,682,050 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi 90,957,997.85 zimekusanywa na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

### Chuo cha Utawala wa Umma

48. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2021, Chuo cha Utawala wa Umma kupitia programu

ya mafunzo mafupi yanayotolewa katika chuo hicho kimetoa mafunzo elekezi kwa Watumishi wapya 1,723 kutoka katika Wizara na Taasisi za Umma Unguja na Pemba kuhusiana na Sheria ya kazi nambari 11 ya Mwaka 2005, Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2014, Maadili ya Utumishi wa Umma, Usalama na Afya kazini, Masuala ya Ulemavu na Fursa za Benki ya Posta kwa Watumishi.

Kwa upande wa programu ya mafunzo ya muda mrefu, jumla ya wanafunzi 1,195 wamepatiwa mafunzo katika ngazi mbali mbali, kati ya hao, 838 ni wanawake sawa na asilimia 70 na 375 ni wanaume sawa na asilimia 30.

**49.** **Mheshimiwa Spika,** watumishi watano (5) wa chuo wamejengewa uwezo katika ngazi zifuatazo: watumishi watatu (3) ngazi ya uzamivu katika fani ya utawala, Ununuzi na Ugavi, Utawala wa Biashara na Uhasibu;  na watumishi wawili (2) ngazi ya Uzamili katika fani za TEHAMA na Mawasiliano kwa Umma. Aidha, watumishi 55 wa Chuo wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya Rasilimali Mtandao katika kusoma, kufundishia na kufanyia tafiti, udahili na uhakiki wa ubora wa viwango pamoja na mfumo wa mitihani na 48 wamepatiwa mafunzo ya "Competence Based Education and Training".

**50. Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa kutumia ruzuku ya Shilingi 1,119,100,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 1,167,084,000 sawa na asilimia 104 zimepatikana kwa ajili ya matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo. Aidha, Chuo kimekadiria kukusanya Shilingi 1,756,360,000 kutokana na malipo ya ada za wanafunzi. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 943,291,370 zimekusanywa sawa na asilimia 54.

**Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

**51. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi 2021 Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kupitia programu ya kusimamia maadili ya viongozi wa umma imehakiki taarifa za mali na madeni za viongozi wa umma 167, sawa na asilimia 84 ya shabaha iliyopangwa. Aidha, jumla ya malalamiko manane (8) ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi kuhusu matumizi mabaya ya madaraka, mgongano wa kimaslahi, unyanyasaji na uonevu yamepokelewa na kufanyiwa kazi.

Vile vile, siku ya Maadili na Haki za Binaadamu yenye kauli mbiu ya "Tuimarishe utoaji wa huduma kwa jamii kwa kuzingatia Maadili, kuheshimu Haki za Binaadamu na kupambana na Rushwa" imeadhimishwa tarehe 29/12/2020. Aidha, Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Tume kwa Mwaka 2019/2020 imeandaliwa na

kuwasilishwa kwa wakati katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa mwezi Februari 2021.

**52. Mheshimiwa Spika,** mafunzo ya kitaalamu ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni kwa Viongozi wa Umma na mafunzo ya Maadili ya Viongozi wa Umma yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa Viongozi wa Umma yametolewa kwa Watumishi wa Tume.

Kwa upande wa uelimishaji jamii, jumla ya vipindi 3 na tangazo la mchezo wa kuigiza kuhusu majukumu ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma na wajibu wa Viongozi wa Umma na wananchi katika kuimarisha maadili vimeandaliwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC).

**53. Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 1,015,000,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 348,485,181 zimepatikana sawa na asilimia 31.5 kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

## A02- AFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI

### Programu ya Uratibu wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi

**54. Mheshimiwa Spika**, kupitia programu hii Afisi ya Baraza la Mapinduzi, imeendelea na usimamizi wa uundwaji wa Serikali mpya ya Awamu ya

Nane kufuatia kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020. Afisi imeandaa kwa ufanisi vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake ikiwemo Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu (*Inter Ministerial Technical Committee – IMTC*). Katika vikao hivyo, pamoja na mambo mengine, nyaraka mbalimbali zikiwemo za Sera na Sheria zimewasilishwa, kujadiliwa na kutolewa uamuzi.

Aidha, Afisi imeratibu vikao kati ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na watendaji Wakuu wa Wizara na Taasisi za umma kujadili utekelezaji wa Mipango kazi ya Wizara na Taasisi hizo.

Vile vile, Afisi imeendeleza programu za kujenga uwezo kwa watumishi kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kwenda sambamba na mabadiliko ya wakati na kuongeza ufanisi wa kazi.

**55.** **Mheshimiwa Spika**, programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 2,237,600,000. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya 1,445,812,465 sawa na asilimia 65 zimepatikana kwa matumizi ya mshahara na kazi za kawaida.

**Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria**

**56.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara iliendelea kuratibu jukumu la utoaji wa huduma ya msaada wa

kisheria kwa wananchi. Kupitia programu hii, Idara ya Msaada wa Kisheria imekamilisha uandaaji wa rasimu ya Kanuni za Malipo ya Wakili na Vakili katika kusimamia kesi za jinai zenye lengo la kurahisisha upatikanaji wa uwakilishi Mahakamani kwa watu wasiokuwa na uwezo. Idara imesajili katika mfumo wa kielektroniki wa watoa huduma za msaada wa kisheria 37 na kupelekea idadi ya waliosajiliwa wote kufikia 143 Unguja na Pemba.

Aidha, Idara kwa kushirikiana na Jumuiya za Wasaidizi wa Sheria imesimamia mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu msaada wa kisheria wafanyabiashara wadogo wadogo na utoaji elimu ya usajili wa ardhi kupitia sanaa kwenye maeneo ya soko na mkutano wa wazi kwa wananchi wa Shehia tatu (3) za Wilaya ya Magharibi 'A' ambazo ni Mtofaani, Hawaii na Mchikichini. Idara pia, imefanya matayarisho ya awali ya Jarida la Msaada wa Kisheria na kupendekeza muundo wa Jarida hilo.

57. **Mheshimiwa Spika,** Idara imefanikiwa kusambaza daftari la watoa huduma za msaada wa kisheria katika Shehia 259 na vituo vya Polisi 13 na kufuatilia taasisi za watoa huduma za msaada wa kisheria 11 Unguja na Pemba. Idara pia, imefanikiwa kuwafikia wananchi 102,838 (wanawake 56,195 na wanaume 46,643) na kuwapatia huduma za msaada wa kisheria zikiwemo ushauri, msaada na elimu ya kisheria na kupokea malalamiko 11 ya wananchi. Kati ya

malalamiko hayo, mawili (2) ni ya mirathi, moja ukaazi wa mtoto, moja wizi, ardhi manne (4), deni mawili (2) na kufukuzwa kazi moja.

58. **Mheshimiwa Spika**, Idara kwa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imetoa elimu kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha SUZA, Chuo cha Utawala wa umma (IPA) na Chuo cha Amali Mkokotoni kuhusu haki za binadamu, uelewa wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Sheria za umiliki na matumizi ya ardhi.

59. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 280,589,080 na hadi kufikia Machi 2021, jumla ya Shilingi 53,444,000 zimepatikana sawa na asilimia 19 kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

### Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini

60. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza jitihada za usimamizi bora wa Madrasa, Afisi ya Mufti kupitia programu hii imesajili Misikiti 143 na Madrasa 222 na kufanya ukaguzi wa vyuo vya Qur-ani 206 na misikiti 141 kwa ajili ya kushauriana na kuangalia changamoto pamoja na kutoa nasaha na ushauri wa maendeleo ya taasisi hizo. Afisi pia, imepokea na kushughulikia migogoro mitano (5) ya Madrasa na 11 ya misikiti ambapo migogoro yote ya Madrasa imetatuliwa na migogoro miwili (2) ya Misikiti inaendelea kushughulikiwa kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi

(Msikiti wa Omar bin Khatab na Msikiti wa Kimara). Aidha, jumla ya migogoro 310 ya ndoa, 25 huduma za wake na watoto, 58 ya mirithi, ardhi na familia imepokelewa na kupatiwa ufumbuzi.

61. **Mheshimiwa Spika,** vikao vitatu (3) vya kuthibitisha kuandama kwa mwezi vimefanyika kati ya vikao saba (7) vilivyopangwa kufanyika katika kipindi hicho. Kadhalika, masuala 555 yalioulizwa kuhusu ndoa, talaka, mirathi, malezi ya watoto, zaka na watu kupotea baharini yamejibiwa. Vipindi 215 vimerushwa hewani kuhusu masuala muhimu katika jamii yetu kwasasa ikiwemo malezi ya watoto, Korona, utaratibu wa kukagua wagonjwa, umuhimu wa Amani, udugu wa kiislamu, jukumu la walimu kwa vijana, utukufu wa mwezi wa Muharam, tatizo la upigaji wanafunzi na udhalilishaji katika madrasa, mmong'onyoko wa maadili, sunna ya aquqah kwa watoto, athari za liwati, kisa cha Israa na Miraji, hukmu ya kiapo katika Uislamu na malezi ya Watoto. Jumla ya masuala 27 yamejibiwa kupitia ZBC Redio.

62. **Mheshimiwa Spika,** wananchi 780 wamehitimu mafunzo ya ndoa na kupewa vyeti, kati ya hao, wanaume 484 na wanawake 296 na jumla ya fatwa 147 zimekusanywa na kuandikwa pamoja. Vile vile, Afisi ya Mufti kwa kushirikiana na Shirika la "Save the Children" imetoa mafunzo kuhusu athari zinazopatikana katika ndoa za umri mdogo kwa baadhi ya Makhatibu wa Misikiti ya Ijumaa Zanzibar, kufanya mikutano na viongozi wa dini kutoka Taasisi mbali mbali za Zanzibar kuhusu

Amani Endelevu kwa Maendeleo Endelevu kwa kushirikiana na Taasisi ya Marafiki wa Zanzibar (The friends of Zanzibar).

**63.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi 932,682,320 na hadi kufikia Machi 2021, jumla ya Shilingi 257,679,769 zimepatikana sawa na asilimia 28 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

## E04: OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

### Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa fedha na Rasilimali za Umma

**64.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia programu hii imekamilisha ukaguzi wa mapato na matumizi kwa Wizara zote za Serikali, Taasisi na Miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo kwa mwaka 2018/2019 na tayari Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imewasilishwa katika mkutano wa Baraza la Wawakilishi wa mwezi Februari 2021. Aidha, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ipo katika hatua za mwisho za kukamilika.

**65. Mheshimiwa Spika,** Afisi imewamepatia mafunzo ya ukaguzi yakinifu, ukaguzi wa kiuchunguzi (Forensic Audit) na mafunzo ya viwango vya ukaguzi vya kitaifa na kimataifa watumishi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao ya ukaguzi. Kwa upande wa mafunzo ya muda mrefu jumla ya watumishi 15 wanaendelea na masomo katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi.

**66. Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 4,243,300,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 3,077,616,800 zimepatikana sawa na asilimia 72.52 kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

## EO5: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI

### Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.

**67. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar imeendelea na jitihada za kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi kwa kuzingatia Sheria namba 1 ya mwaka 2012 Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kifungu nambari 13(1). Jitihada hizo zinahusu kufanya uchunguzi juu ya tuhuma za rushwa kwenye sekta ya umma, mashirika na sekta binafsi na kuchukua hatua.

Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya tuhuma 316 za makosa mbali mbali ikiwemo kuomba na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya Afisi, Ubadhirifu wa mali na mapato, kukwepa kulipa kodi, kumdanganya muajiri, kusafirisha magendo, mgongano wa maslahi, rushwa katika uchaguzi na rushwa katika zabuni zimeripotiwa na kushughulikiwa katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kupitia programu ya Uzuiaji Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. Kati ya tuhuma hizo, 228 zinaendelea na uchunguzi, 57 zimefungwa na tuhuma 13 zimehamishiwa katika taasisi nyengine. Aidha, tuhuma 29 zimetolewa ushauri, 13 zimefanyiwa udhibiti na tuhuma 23 uchunguzi wake umekamilika na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa ajili ya kuombewa kibali cha kuwasilishwa Mahkamani na tuhuma 3 zimetolewa hukumu. **(angalia kiambatisho namb. 5b).**

**68. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki, Shilingi 432,585,724 zimeokolewa kutokana na operesheni mbali mbali za uchunguzi na ufuatiliaji wa makosa ya Rushwa na uhujumu wa uchumi. Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika Miradi ya maendeleo nchini unaendelea ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha inapatikana.

**69. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kuelimisha jamii kuhusu athari na madhara ya rushwa na uhujumu uchumi kupitia mikutano

mbali mbali ya Shehia, Klabu za wapinga Rushwa katika shule za Sekondari, mikutano ya Afisi za umma na binafsi, vipindi vya redio na televisheni, machapisho na kushiriki katika maonyesho mbali mbali ya biashara.

**70.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 2,108,400,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 1,230,284,642 zimepatikana sawa na asilimia 58 kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

## E07: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

### Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma

**71.** **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utumishi wa Umma ina jukumu la kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma yanasimamiwa na kuendeshwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu mbalimbali. Aidha, Kamisheni ni Mamlaka ya Rufaa kwa Watumishi wa Umma dhidi ya Uamuzi unaotolewa na mamlaka zao za nidhamu.

Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, kupitia programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma, Kamisheni imeendelea kufanya ukaguzi maalum katika Mashirika ya Umma 12, Wakala Tendaji 2 na Taasisi zinazojitegemea 2 kwa upande wa Unguja kwa lengo la kuangalia kiwango cha uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na

Taratibu za Utumishi wa Umma katika utoaji wa huduma. Ukaguzi huu utaendelea kwa upande wa Pemba pia. Aidha, Kamisheni ya Utumishi wa Umma imechambua na kuridhia Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi 14 za Umma, kupokea na kushughulikia Rufaa sita (6) za kiutumishi kutoka kwa watumishi wa umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka zao za Ajira na Nidhamu katika Utumishi wa Umma na kutoa uamuzi.

Vile vile, Kamisheni imeandaa na kuwasilisha kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Kamisheni Kifedha na kuandaa Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2018/19 na kuiwasilisha Baraza la Wawakilishi.

Kwa upande wa mafunzo ya watumishi, jumla ya Watumishi sita (6) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi wanne (4) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 1,276,100,000 hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 501,157,248 zimepatikana sawa na asilimia 39.3 kwa malipo ya mishahara na matumizi mengineyo.

## E08: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

### Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini

**73. Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii Tume ya Utumishi Serikalini imetangaza nafasi mbali mbali za ajira, kufanya usaili na kutoa kibali cha ajira ya nafasi 3,280 za Watumishi wa kudumu katika fani tofauti kwa Wizara/Idara mbali mbali za Serikali Unguja na Pemba. Kati ya hizo, nafasi 2,429 za ajira zilitolewa kwa upande wa Unguja, wanawake 1,612 na wanaume 817. Kwa upande wa Pemba nafasi 851 zimetolewa, wanawake 481 na wanaume 370**. (angalia kiambatanisho namb. 6a)**

**74. Mheshimiwa Spika,** Tume imewathibitisha kazi watumishi 1,317, kuwapandisha daraja watumishi 622, kuwabadilisha kada watumishi 58 na kuidhinisha nyongeza za muda wa utumishi kwa watumishi 7. Watumishi 315 wamestaafishwa kazi kwa kutimiza umri wa kustaafu kwa lazima, 26 wamestaafu kazi kwa hiari na watumishi saba (7) wamestaafishwa kazi kwa maradhi. Aidha, Tume imeidhinisha uajiri wa mkataba kwa watumishi 13, kuridhia kuacha kazi kwa watumishi saba (7) na mtumishi mmoja kuchukua likizo bila malipo. **(angalia kiambatanisho namb. 6b.)**

**75. Mheshimiwa Spika,** malalamiko manne (4) kuhusu masuala ya kinidhamu yamepokelewa

na kushughulikiwa ambapo lalamiko moja limetolewa uamuzi, moja linaendelea kufanyiwa kazi na mawili yaliosalia yamehamishiwa katika sehemu husika nyengine. Katika kipindi hiki, watumishi 35 wameombewa kibali cha kufukuzwa kazi kutoka kwa Mamlaka zao za nidhamu baada ya kuthibitika kuwa wamefanya makosa ya kinidhamu katika sehemu zao za kazi ambapo maombi hayo bado yanaendelea kushughulikiwa. **(angalia kiambatanisho namb. 6c.)**

**76. Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 640,000,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 301,418,000 zimepatikana sawa na asilimia 47 kwa matumizi ya mshahara na matumizi mengineyo.

## G02: MAHKAMA KUU

### Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki

**77. Mheshimiwa Spika,** Mahakama ya Zanzibar imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutafsiri sheria, kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri yote ya jinai na madai yanayowasilishwa katika ngazi zote za mahkama ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki kwa wakati kupitia programu ya usimamizi na upatikanaji wa haki.

Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Mahkama imepokea na kusajili jumla ya kesi 7,507 kutoka mahkama zote za Unguja na Pemba. Kati ya hizo, kesi 4,485 zimesikilizwa na kutolewa uamuzi sawa na asilimia 60.

Katika usajili huo, Mahkama Kuu pekee imesajili mashauri mapya 181 na hadi kufikia mwezi Machi 2021, mashauri 17 yametolewa uamuzi sawa na asilimia 99. Kitengo cha Mahkama ya Kazi kimepokea na kusajili maombi 27 na hadi kufikia mwezi Machi 2021 maombi 2 yametolewa uamuzi sawa na asilimia 7.4. Mahkama ya Biashara imepokea mashauri ya madai mapya 3 ukijumuisha na mashauri 10 ya nyuma na kuwa na jumla ya mashauri 13, mashauri hayo yapo katika hatua mbali mbali za kusikilizwa. Katika Mahkama za Mkoa, mashauri mapya 886 yamepokelewa na hadi kufikia mwezi Machi 2021 mashauri 97 yametolewa uamuzi sawa na asilimia 11.

78. **Meshimiwa Spika,** hatua za usikilizwaji wa kesi kwa mahkama zilizosalia ikiwemo mahkama ya Kadhi, Wilaya na rufani ni kama inavyoonekana katika **(kiambatisho namb. 7a, b na c)**

Kwa upande wa kesi za udhalilishaji Mahkama maalumu ya kushughulikia kesi za udhalilishaji imeanza kusajili rasmi kesi za udhalilishaji kuanzia tarehe 9/02/2021 ambapo imepokea na kusajili kesi 168 kati ya hizo, kesi 3 zimetolewa uamuzi.

79. **Mheshimiwa Spika,** vikao vya pamoja na wahusika wote wa haki jinai vimefanyika ambapo masuala ya Madawa ya kulevya na kesi za Udhalilishaji na mengineyo yamejadiliwa. Vile vile, Mahkama imeadhimisha kilele cha siku ya Sheria tarehe 09/02/2021 yenye kauli mbiu "Wajibu wa Mahkama na wahusika wa Sheria kwa kuendana na kasi ya Awamu ya Nane katika kushughulikia kesi". Mgeni rasmi katika madhimisho hayo alikuwa Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

80. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 7,926,200,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 3,680,528,854 zimepatikana sawa na asilimia 69 kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo. Mahkama ya Kadhi imepokea ruzuku ya Shilingi 761,482365 sawa na asilimia 92 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Aidha, jumla ya Shilingi 356,560,759 zimekusanywa na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 60.

**G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU**

**Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa huduma za Sheria**

81. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi 2020/2021 Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza jukumu la msingi la kuhakikisha kwamba Sheria za nchi

zinakwenda na wakati na zinakidhi haja ya kisera na vipaumbele vya Serikali. Kupitia programu hii, Miswada mitano (5) iliwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi ambayo ni Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2021; Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA ya mwaka 2020; Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Chuo cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano wa mwaka 2020; Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi ya mwaka 2020; na Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya mwaka 2020 wa Mwaka 2021. Aidha, jumla ya Kanuni 17 zinazotokana na Sheria tofauti zimeandaliwa kwa lengo la kuzifanya Sheria hizo ziweze kutekelezwa kwa ufanisi zaidi na kuandaa Matangazo ya kisheria 116 kuhusu mambo mbali mbali na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. **(angalia kiambatanisho namb. 8)**

**82.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara, mashirika ya umma na taasisi zinazojitegemea. Katika kipindi hiki, rasimu za Mikataba 215 zimefanyiwa mapitio na kutolewa ushauri, kati ya mikataba hiyo, 136 ni ya bidhaa na huduma, 45 ujenzi, 20 ushauri elekezi na 14 ni kuhusu kodi. Aidha, Hati za Maelewano (MoU) 18 kuhusu masuala ya elimu, afya na kilimo zimefanyiwa mapitio na kutolewa ushauri.

Kwa upande wa usimamiaji wa kesi, jumla ya kesi 106 zimesimamiwa katika mahkama mbali mbali. Kati ya hizo, kesi tano (5) zimemalizika na kutolewa hukumu na kesi 14 ni mpya na zinaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, Afisi imepokea na kushughulikia indhari 26 za kuishtaki Serikali.

Hadi kufikia mwezi Machi 2021, jumla ya kesi 49 zinaendelea katika Mahkama za Unguja na Pemba ambapo mbili (2) kati ya hizo, zipo katika hatua ya maelewano na kesi tatu (3) zipo katika hatua ya uamuzi.

83. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 2,273,100,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 999,882,316 zimepatikana sawa na asilimia 44 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

## G04: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

### Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai

84. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kupitia programu ya Usimamizi wa utekelezaji wa kesi imeendesha jumla ya kesi za jinai 2,295 katika mahakama mbali mbali za Unguja na Pemba. Kati ya kesi hizo, 2,254 zimefanyiwa kazi katika mahakama za Wilaya na Mikoa na kesi 41 zimefanyiwa kazi katika Mahkama Kuu. Uendeshaji wa kesi hizo upo katika hatua mbali mbali za usikilizwaji. Vile

vile, Afisi imeimarisha ushirikiano na taasisi nyengine zinazohusika na masuala ya jinai kama vile Mahakama, Magereza, Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ili kuhakikisha usimamizi bora wa haki za jinai kwa wananchi.

Aidha, wafanyakazi wawili (2) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika kada ya sheria ngazi ya shahada ya uzamili (Master Degree in Laws). Jumla ya Wanasheria 10 walihudhuria mafunzo mbali mbali ya muda mfupi kwa ajili ya kuongeza ujuzi na taaluma ya kutekeleza majukumu yao ya kazi.

Kwa upande wa Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar, Afisi imefanikiwa kutoa mafunzo ya sheria ya muda mfupi na muda mrefu kwa ngazi ya cheti na stashahada ya sheria.

**85.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 2,293,912,500. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 1,525,956,563 zimepatikana sawa na asilimia 67. Kati ya hizo, Shilingi 1,277,475,000 kwa ajili ya mishahara na Shilingi 248,481,563 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya shilingi 37,449,184 zimepatikana kwa ajili ya ruzuku sawa na asilimia 27.

## G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

### Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria

**86.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea kuhakikisha kwamba sheria za nchi

zinafanyiwa mapitio na kuimarishwa ili ziendane na wakati kwa kuzingatia mabadiliko ya kijami, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Hadi kufikia Machi 2021, Tume ya Kurekebisha Sheria kupitia programu hii imeendelea kukamilisha mapitio ya Sheria ya kuanzisha Afisi ya Mufti Namba 9, Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya Mwaka 2011 na Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Namba 16 ya Mwaka 1986.

Pia, Tume imepitia Mswaada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri wa Kodi na Mswaada wa Usimamizi wa "Microfinance". Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai Sura ya 8 ya Mwaka 1917 kukamilisha mapitio ya kanuni zake (7). Miongoni mwa Kanuni hizo ni kanuni ya Wadaawa katika Madai, Uandaji wa Madai, Wanaoruhusiwa kufungua madai, Ufunguzi wa Madai, Taratibu za Wito, Hati ya madai na maelezo ya maandishi, Hati ya madai na Majibu ya Madai na suluhu.

**87. Mheshimiwa Spika,** Tume imeendelea na kazi ya kuzitafsiri Sheria ya Pombe ya Kienyeji Sura 164 ya mwaka 1942 (Native Liquor Decree Cap.164), Sheria ya Wazururaji ya Mwaka 1962 (Vagrant Decree No.21 of 1962) na Sheria Namba 4 ya mwaka 2005 ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi mmoja (The Spinsters and Single Parent Children Protection Act No.4 of 2005.

Vile vile, katika kukuza uwelewa wa jamii juu ya kazi za Tume na umuhimu wa Mapitio ya Sheria,

jumla ya vipindi 11 vya Redio na televisheni vimerushwa hewani kupitia Zanzibar Cable Television (ZCT), Bahari FM, na Assalam FM Radio, Majarida mawili yamechapishwa na kopi 1,500 zimesambazwa kwa taasisi na wananchi mbalimbali na kufanya kongamano kuhusu "Amani kabla ya uchaguzi na baada ya uchaguzi" na kuwashirikisha vijana na viongozi wa dini.

88. **Mheshimiwa Spika**, Tume imewajengea uwezo watendaji wake wawili kupitia ziara ya mafunzo ya siku nne Nchini Mauritius kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na watendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria ya Mauritius. Ziara hiyo imesaidia sana katika kupata uzoefu na kuimarisha mashirikiano na Taasisi zinazofanyakazi sawa na Tume. Aidha, wafanyakazi watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mtumishi mmoja mafunzo ya muda mrefu.

89. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii imepangiwa jumla ya shilingi 1,173,500,000. Hadi kufikia Machi 2021, Shilingi 394,197,826 zimepatikana sawa na asilimia 33.5. Kati ya hizo Shilingi 259,253,200 kwa ajili ya mishahara na Shilingi 134,944,626 kwa matumizi mengineyo.

## C. MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

90. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa kutumia fursa hii kutoa maelezo ya muelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

91. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi ya Rais- Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutumia jumla ya Shilingi 55,930,775,000. Kati ya hizo, Shilingi 14,642,100,000 zimepangwa kutumika kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na shilingi 12,756,700,000 zimepangwa kutumika kwa matumizi mengineyo. **(angalia kiambatanisho namb 2).**

92. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imepanga kutumia ruzuku ya Shilingi 5,850,100,000 kwa ajili ya mshahara na matumizi mengineyo ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Chuo cha Utawala wa Umma na Tume ya Maadili ya Viongozi. Kwa upande wa kazi za maendeleo Shilingi 22,681,175,000 zimepangwa kutumika kutekeleza miradi ya maendeleo. Pia, Ofisi imepanga kukusanya jumla ya Shilingi 197,700,000 kuchangia mfuko mkuu wa Serikali **(angalia kiambatanisho namb. 1, 2 &3).**

## D. VIPAUMBELE VYA OFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

93. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuimarisha utendaji katika taasisi za Sheria kwa kufanya marekebisho ya sheria mbali mbali na matengenezo ya majengo ya Mahkama na ofisi;

ii. Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Huduma ya Msaada wa Kisheria;

iii. Kukamilisha na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria wa Awamu ya Pili;

iv. Kuimarisha mfumo wa haki jinai nchini na kukamilisha mfumo wa utoaji huduma hiyo kwa njia ya TEHAMA katika mahkama;

v. Kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma na masuala ya utawala bora;

vi. Kusimamia majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake;

vii. Kuimarisha usalama wa watumishi wa umma na maeneo wanayofanyia kazi;

viii. Kutekeleza Awamu ya Pili ya Mkakati wa Mabadiliko ya Utumishi wa Umma Zanzibar (ZPSRP); na

ix. Kuanza ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar.

**Malengo Makuu ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

**94. Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kuimarisha upatikanaji wa haki na utawala wa sheria;
ii. Kuimarisha utoaji wa huduma za kisheria na usimamizi wa mikataba;
iii. Kuhakikisha upatikanaji wa haki za jinai kwa amani, utulivu na maendeleo ya kiuchumi;
iv. Kuimarisha kazi za marekebisho ya Sheria za nchi ili ziendane na mabadiliko ya mazingira na wakati;
v. Kuongeza uwelewa kwa jamii kuhusu masuala ya rushwa na uhujumu uchumi;
vi. Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa raslimaliwatu katika utumishi wa umma;
vii. Kuimarisha kazi za usimamizi wa haki na nidhamu ya watumishi wa umma;
viii. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Raslimali watu wa mwaka 2021/2022 na Mpango wa Mafunzo ya watumishi wa umma;
ix. Kuimarisha miundo na mifumo ya taasisi;

x. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika shughuli na utoaji wa huduma za Serikali;
xi. Kuimarisha misingi ya utawala bora na maadili katika utendaji wa shughuli za Serikali;
xii. Kuongeza uwelewa wa utunzaji wa siri za Serikali kwa watumishi wa umma.

**95. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha maelezo ya programu za Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ifuatavyo:-

**96. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza Programu kuu 15 kama ifuatavyo: i) Programu ya Usimamizi wa masuala ya Sheria; ii) Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora; iii) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini iv) Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa ARKSUUB; v) Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma vi) Programu ya Huduma za Serikali Mtandao; ziliomo katika fungu **G01**; na vii) Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa haki **G02;** viii)Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria **G03**; ix) Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai **G04**; x) Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria **G05;** xi)Programu ya Uratibu wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi) **A02**; xii) Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma **E04**;

xiii) Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi **E05**; xiv) Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma **E07**; xv) Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini **E08**;

**97.** **Mheshimiwa Spika,** kati programu hizi, programu kuu sita (6) za fungu **G01** zinasimamiwa na kutekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu na Programu zilizobakia zinatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea.

**98.** **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa vipaumbele hivi na malengo na mpango wa bajeti utazingatia Dira ya Mendeleo ya Zanzibar ya 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025, Ahadi za Mheshimiwa Rais alizozitoa wakati wa kampeni ya uchaguzi wa Oktoba 2020, hotuba ya Mheshimiwa Rais alioitoa wakati wa uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi na maagizo ya Serikali yaliotolewa wakati wa hafla ya kuwaapisha Mawaziri na Makatibu Wakuu Ikulu Zanzibar.

***G01- Afisi ya Rais- Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora***

***Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria.***

**99.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu ya Usimamizi wa Msaada

wa Kisheria imepanga kutoa elimu ya sheria kwa wananchi kupitia maadhimisho ya wiki ya msaada wa sheria; kuwajengea uwezo Maafisa wa Idara ya Msaada wa Sheria kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi; kuandaa ripoti ya mwaka ya msaada wa kisheria na kuchapisha; kuandaa mikutano ya uratibu ya robo mwaka ya wahusika wa msaada wa kisheria; na kuimarisha uhusiano wa kitaifa na kikanda kwa watoa huduma za msaada wa kisheria.

**100. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 204,071,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

***Programu ya Usimamizi wa Masula ya Dini.***

**101. Mheshimiwa Spika,** Programu hii itaendelea kusimamia Misikiti, Madrasa na kutoa miongozo ya Walimu wa Madrasa katika dini ya Kiislamu; kushughulikia na kutatua migogoro katika familia, misikiti na madrasa pamoja na kutoa mafunzo ya wanandoa wapya katika ngazi ya Wilaya zote. Programu hii pia, itaratibu maandalizi ya utekelezaji wa sala na Mabaraza ya Eid kitaifa.

Aidha, vikao vya kuandama kwa mwezi na vikao vya Baraza la Ulamaa vya kila mwezi vitaendelea kufanyika na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya dini ya kiislamu kupitia vyombo vya habari

pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wa ofisi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

**102.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 879,094,868.20 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

***Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora.***

**103.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu ya usimamizi wa utawala Bora imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: kuijengea uwezo jamii kuhusu majukumu ya kijamii na kuongeza uelewa wa utawala bora kwa viongozi wakuu; kuwajengea uwezo Walimu wa somo la uraia na kuandaa Mtaala wa elimu ya uraia; kujenga uelewa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu masuala ya utawala bora na kuziendeleza klabu za utawala bora za wanafunzi; kutayarisha Jarida la Utawala Bora; kutunga Sheria ya Usimamizi wa Utawala Bora na kuanzisha Mpango wa pamoja wa kusimamia utekelezaji wa misingi ya utawala bora; na Kufanya tathmini ya utawala bora.

**104.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 253,317,443 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

***Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma.***

**105. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma ina programu ndogo mbili zinazotekelezwa kupitia Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi.

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu ndogo ya Mipango na Maendeleo ya Watumishi inayotekelezwa na Idara ya Mipango Rasilimali Watu imepanga kutekeleza na kusimamia Mpango wa Rasilimali Watu wa mwaka 2022/2023 katika Utumishi wa Umma, kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Taasisi za Umma na upatikanaji wa mafunzo yanayotolewa na Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kuongeza fursa za mafunzo kwa watumishi wanaohitaji kujiendeleza. Aidha, kupitia programu hii, Idara itaendelea kuratibu mafunzo ya Wastaafu katika Utumishi wa Umma na kuendelea na matayarisho ya Mpango Mkakati wa Sera ya Mafunzo kwa Watumishi wa Umma pamoja na kuhakiki taarifa za watumishi wa Umma.

**106. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 338,261,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

**107. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu ya Miundo na Mifumo ya Taasisi inayotekelezwa na Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi itafuatilia utekelezaji wa Mkataba wa utoaji wa Huduma kwa Mtaka Huduma, zoezi la upimaji utendaji kazi pamoja na Muundo wa Utumishi kwa Wizara, Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea. Aidha, Idara itafanya mapitio ya kazi na majukumu kwa Wizara na Taasisi za Serikali, kuendeleza kazi ya uhakiki wa malipo ya mishahara na Posho kwa Wizara, Mashirika, Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea na kuadhimisha Siku ya Utumishi Zanzibar.

**108. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 350,977,868.78 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

### *Programu ya Huduma za Serikali Mtandao*

**109. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kupitia programu hii, Wakala wa Serikali Mtandao itaendelea kuimarisha Mazingira ya utendaji kazi na shughuli za uendeshaji wa Wakala ili iweze kutoa huduma bora za Serikali Mtandao.

Katika kipindi hiki, Wakala imepanga kufanya mapitio ya Sera na Mpango Mkakati wa Serikali Mtandao na kuandaa kanuni za TEHAMA kwa mujibu wa Sheria ya Wakala na kufanya vikao vya wahusika mbali mbali wa TEHAMA. Aidha, Wakala itaandaa Mkataba wa Huduma kwa wateja na kutoa miongozo mbali mbali ya usimamizi wa masuala ya TEHAMA.

**110. Mheshimiwa Spika,** nyaraka za kitaalamu za uanzishwaji wa miradi ya TEHAMA katika utumishi wa umma zitaendelea kufanyiwa mapitio na kufanya tathmini na ukaguzi wa Mifumo na vifaa vya TEHAMA katika Taasisi za Umma pamoja na kuandaa mifumo ya kieletroniki ya utoaji wa huduma.

**111. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 659,366,172.62 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

***Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ARKSUUB***

**112. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo nne (4) zinazotekelezwa kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Usalama wa Serikali na Afisi Kuu- Pemba.

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, programu ya Uendeshaji na Utawala wa Afisi inayotekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi itaendelea kusimamia nidhamu na kulipa stahiki za watumishi, kutoa huduma za uendeshaji na kufanya matengenezo ya Afisi na vifaa.

Aidha, kupitia programu hii, Idara itaendelea na tathmini ya utendaji kazi na kufanya zoezi la tathmini ya uwezo wa Watumishi (Capacity Needs Assessment) na kusimamia Mfumo wa Taarifa za watumishi na mfumo wa usimamizi wa fedha. Vile vile, Idara itasimamia utekelezaji wa Mpango wa ununuzi na kufanya vikao vya Bodi ya zabuni; kutekeleza Mpango wa Ukaguzi wa Hesabu wa ndani na kufanya vikao vya Kamati ya Ukaguzi; na kufanya mapitio ya Mpango wa Rasilimali Watu wa Wizara wa miaka mitano. Aidha, Idara itaendelea kuripoti matukio mbalimbali ya Wizara katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii na kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara.

**113.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 1,016,586,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

**114.** **Mheshimiwa Spika,** programu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti itaendelea kuratibu na kuandaa sera, mipango na bajeti ya Afisi na utekelezaji wa miradi ya Sekta ya Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Kupitia programu

hii, Idara itaratibu na kufanya mapitio ya Sera na Sheria za Sekta ya Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kushirikiana na taasisi husika pamoja na kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Afisi na kufanya tafiti. Vile vile Idara itaratibu uanzishwaji wa Skuli ya Sheria.

**115.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 296,918,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2).**

**116.** **Mheshimiwa Spika,** programu ya Usimamizi wa usalama wa watumishi inayotekelezwa na Idara ya Usalama wa Serikali imepanga kufanya upekuzi wa kiusalama wa Awali na Endelevu kwa Watumishi wa Umma wanaotarajiwa kuajiriwa katika Serikali na watumishi wanaotarajiwa kupandishwa vyeo. Idara itafanya ukaguzi wa kiusalama wa Majengo na Miundombinu ya Afisi za Serikali na kutoa ushauri wa kufaa ili kuimarisha mazingira na usalama wa afisi za Serikali pamoja na kutoa mafunzo ya utunzaji wa siri na udhibiti wa nyaraka kwa watumishi wa umma.

**117.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 285,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

**118. Mheshimiwa Spika,** programu ya Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Afisi Kuu Pemba itaendelea kuratibu na kusimamia shughuli zote za utawala na utumishi, mipango na bajeti zinazotekelezwa na Afisi kwa upande wa Pemba.

**119. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 781,671,433 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

***TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU- G01***

***Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana***

**120. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana itaendelea kutoa huduma za Mirathi kwa njia ya kieletroniki, kutumia nidhamu ya zakka katika utoaji wa hifadhi ya jamii na kuimarisha huduma za Wakfu na Amana katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Vile vile, Kamisheni itaendelea na utoaji wa huduma za Hijja na Mfuko wa Hijja ili wananchi waweze kutekeleza wajibu wao pamoja na kukusanya Zakka na misaada ya kheri.

**121. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla

ya Shilingi 1,267,200,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

### *Chuo Cha Utawala wa Umma*

**122. Mheshimiwa Spika,** Chuo Cha Utawala wa Umma kupitia programu za mafunzo mafupi na muda mrefu kimepanga kuendesha mafunzo ya kujenga uwezo wa watumishi wa umma na kutoa mafunzo elekezi kwa watumishi wapya wanaoongia katika ajira kwa mara ya kwanza ili kuondoa upungufu na mahitaji katika sekta za umma. Chuo kitafanya tafiti mbali mbali za kubaini upungufu na mahitaji yaliyopo katika sekta ya umma na kutoa huduma ya ushauri elekezi kwa taasisi hizo.

Aidha, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wa umma na wananchi katika ngazi ya Shahada, Stashahada na Astashahada kwa ajili ya kuiwezesha Serikali kujitegemea na kuwa na wataalamu wake.

**123. Mheshimiwa Spika,** ili kukiwezesha Chuo kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya Shilingi 1,503,500,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Aidha, Chuo kimepanga kukusanya Shilingi 2,024,415,000 kutokana na malipo ya ada za wanafunzi **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

### *Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma*

**124. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2021/2022 itaendelea kupokea, kuhifadhi na kuhakiki taarifa za mali na madeni ya viongozi wa Umma kwa njia ya kielektroniki, kuelimisha viongozi wa umma juu ya umuhimu wa kuzingatia maadili katika utekelezaji wa majukumu yao ya uongozi. Aidha, Tume inatarajia kukusanya fomu za tamko la rasilimali na madeni kutoka kwa viongozi wa umma na kuzifanyia kazi pamoja na kupokea malalamiko ya uvunjwaji wa Sheria ya Maadili na kufanya uchunguzi.

**125. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 1,151,300,000 kwa matumizi ya kawaida **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

### *A02: AFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI*

### *Programu ya Uratibu wa Majukumu Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi.*

**126. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo mbili zifuatazo; programu ya Uratibu wa Shughuli za Baraza la Mapinduzi na ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji kazi wa Taasisi za Umma.

**127.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria ya kuratibu na kusimamia shughuli za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake zikihusisha kuandaa mikutano yake pamoja ka kutunza kumbukumbu zake, kufanya uchambuzi wa nyaraka zinazowasilishwa katika Baraza la Mapinduzi na Kamati zake, kuwasilisha maamuzi na maelekezo ya Baraza la Mapinduzi kwa taasisi zinazohusika na kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera, Sheria, Miongozo na Maagizo mbalimbali yanayotolewa na Serikali.

**128.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 2,194,500,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

***G02: MAHKAMA KUU***

***Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki***

**129.** **Mheshimiwa Spika,** 2021/2022, Mahkama itaendelea na utekelezaji wa jukumu la kupokea na kusikiliza kesi na kutoa uamuzi kwa wakati, kuhakikisha mfumo wa kisasa wa kuendesha na kurikodi kesi unaimarika na kukumilisha ujenzi wa Jengo la Mahkama Kuu Tunguu na kufanya matengenezo ya majengo ya Mahkama Unguja na Pemba.

**130. Mheshimiwa Spika**, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 8,246,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo, Mahkama Kuu shilingi 7,008,900,000 na Mahkama ya Kadhi shilingi 1,237,100,000. Aidha, Mahkama ya Kadhi imepangiwa kukusanya shilingi 869,919,000 **(angalia kiambatanisho namb. 2 &3)**

***G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU***

***Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa huduma za Sheria***

**131. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia programu hii itaendelea na kuiwakilisha Serikali dhidi ya kesi zote za madai na kufanya uchambuzi wa masuala mbali mbali ya kesi za madai na uandaaji wa miswada. Afisi itaendelea kusimamia na kutoa ushauri wa Mikataba ambayo Serikali inatarajia kuingia na kutoa elimu ya kisheria kwa jamii. Aidha, Afisi itawajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya masuala ya uendeshaji kesi, uandaaji wa miswada na usimamizi wa mikataba ili waweze kusimamia majukumu yao kwa ufanisi. Pia, kujenga mashirikiano ya kikazi baina ya watendaji wa SMZ na SMT ili kuleta tija katika umma.

**132. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 2,398,700,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

### *G04: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA*

### *Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai*

**133. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022**,** Afisi ya Mkurugenzi wa Mashataka itaendelea kuendesha kesi katika Mahkama za Wilaya, Mkoa na Mahkama za watoto Unguja na Pemba. Afisi pia, itawajengea uwezo wa kiutendaji Waendesha Mashtaka ili waweze kutekeleza majukumu yao ya uendeshaji wa kesi mahkamani, kukiendeleza Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti na kuendelea kuratibu shughuli za upelelezi.

**134. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 2,786,900,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na ruzuku ya Shilingi 197,700,000 kwa ajili ya Kituo cha Mafunzo ya Sheria **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

### *G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA*

### *Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria*

**135. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Tume ya Kurekebisha Sheria kupitia programu hii imepanga kufanya mapitio ya Sheria ya Uvuvi Nam. 7/2010 (The Fisheries Act 7/2010), Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia Nam. 6/2016 (The Oil and Gas (Cupstream) Act 6/2016, Sheria ya Kuanzisha Chuo cha Mafunzo nam. 1 ya Mwaka 1980 (The Offenders Education Act No.1 of 1980), Sheria ya Zimamoto na Uokozi Act Nam. 7 ya 1999 (Fire brigade Act. No. of 1999) na Sheria ya Kikosi cha Valantia Nam.5 ya 2004.

Tume itatafsiri katika lugha nyepesi ya Kiswahili Sheria 4 ili ziweze kufahamika vizuri na wananchi, kufanya utafiti na kukusanya Sheria za Zanzibar na kuandaa ripoti. Aidha, utendaji wa Tume utaimarishwa kwa kushirikiana na Taasisi zenye majukumu sawa na Tume kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kuwapatia watendaji wake mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuongeza ufanisi na utendaji kazi katika majukumu yao ya kila siku. Vile vile, Tume itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vipindi vya redio na Televisheni, makongamano na semina.

**136. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, tunaiomba Kamati yako iidhinishe jumla ya Shilingi 2,956,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

### *E04: AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI*

### *Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Raslimali za Umma*

**137. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022, itaendelea kufanya majukumu yake ya kikatiba ya kukagua hesabu za Serikali na Taasisi zake zote kwa kutumia viwango vya Ukaguzi vya kitaifa na kimataifa pamoja na kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi. Afisi itakamilisha ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2019/2020 na kuwasilisha katika mamlaka husika.

**138. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 4,170,200,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

### *E05: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI*

### *Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi*

**139. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kwa mwaka wa fedha

2021/2022, itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu athari na madhara ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, kufanya uchunguzi wa tuhuma na makosa ya rushwa na uhujumu wa uchumi, kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wake na kufuatilia matumizi ya fedha za Umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha.

Aidha, Mamlaka itaandaa Taarifa ya Hali ya Rushwa ya Mwaka 2021 na kuiwasilisha katika Mamlaka husika na kufanya marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Na. 1 ya mwaka 2012.

**140.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 2,159,100,000 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 20,950,000,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

### *E07: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA*

### *Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma*

**141.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2021/2022 Kamisheni itaendelea kufanya Uchambuzi wa Miundo ya Taasisi, Miundo ya Utumishi na Miundo ya Mishahara kumi na mbili (12) itakayowasilishwa Kamisheni; kufanya mapitio ya Matoleo ya Miundo na kuandaa Muongozo

wa Nidhamu. Kamisheni pia, itafanya zoezi la tathmini ya utekelezaji wa Miundo iliyoidhinishwa na Kamisheni katika Taasisi za Umma.

142. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni itafanya ukaguzi wa kawaida katika taasisi za umma 32, ukaguzi maalumu katika taasisi nne (4) na ukaguzi wa kushtukiza katika taasisi za umma nne (4) Unguja na Pemba. Aidha, itapokea na kushughulikia rufaa 12 kutoka kwa watumishi na mamlaka za nidhamu, kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini katika Utumishi wa Umma na Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2020.

143. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 1,364,300,00 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

***E08: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI***

***Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini***

144. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utumishi Serikalini kwa mwaka wa fedha 2021/2022, itathibitisha na kusimamia shughuli za ajira, haki na nidhamu za watumishi, kutoa vibali vya kustaafu kwa watumishi waliofikia umri wa kustaafu, kupandisha daraja, kubadilisha kada na kuidhinisha likizo bila ya malipo kwa

watumishi wa Serikali. Aidha, mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi yatatolewa kwa watumishi wake ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**145.** **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 48,600,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho namb. 2)**

## E. SHUKRANI

**146.** **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 katika utekelezaji wa majukumu yetu. Napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia katika kutekeleza programu na mipango yetu ya uimarishaji sekta ya Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuleta maendeleo kwa wananchi. Naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni: - Jamhuri ya Watu wa China, India, Saudi Arabia, Oman na Malaysia. Vile vile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni:- Benki ya Dunia (World Bank), Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IDB), Benkji ya Maendeleo ya Afrika (AfDB),Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo ya

Kimataifa (UNDP), Legal service Facility (LSF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuzuia Uhalifu na Madawa ya Kulevya (UNODC), Shirika la Umoja wa Matifa la Kupambana na Vitendo vya Rushwa (UNCAC) na Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma (AAPAM).

**147. Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena nawashukuru viongozi wenzangu na nikianza na Nd. Seif Shaaban Mwinyi, Katibu Mkuu, Nd. Mansura Mosi Kassim Naibu Katibu Mkuu; Makamishna na Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza malengo na majukumu ya Ofisi hii ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru waajiri na watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi na uzalendo wa hali ya juu katika kuwahudumia wananchi. Vile vile, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Katiba na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vyombo vya Sheria vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Rais, Idara Kuu ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mamlaka ya Serikali Mtandao ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Taasisi ya Makatibu Muhutasi Tanzania (TAPSEA) na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) na Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA).

